# Ijue Sengerema

TOLEO NAMBA 02 JANUARI HADI MACHI 2023


LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI CHA HALMASHAURI WA WILAYA YA SENGEREMA www.sengeremadc.go.tz Email: ded@sengeremadc.go.tz



**MIAKA MIWILI MADARAKANI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**

## SENGEREMA

**INASONGA MBELE**











## PONGEZI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWA MIAKA MIWILI MADARAKANI

## SENGEREMA KAZI INAENDELEA



# BARAZA LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 56

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema tarehe 10 Januari, 2023 limepitisha mapendekezo ya mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024 yenye kiasi cha shilingi 56,136,022,839.00 (Bilioni hamsini na sita, milioni miamoja thelathini na sita, elfu ishirini na mbili na mia nane thelathini na tisa bila senti) huku likisisitiza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Katika kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Yanga Makaga ameiagiza timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuhakikisha inaweka mikakati madhubuti ya ukasanyaji wa mapato kwani bajeti pendekezwa kwa upande wa mapato ya ndani imeongezeka kwa asilimia 18 kutoka shilingi 2,749,992,000 ya mwaka 2022/2023 na kufikia shilingi 3,377,319,839.00.
"ongezeko la asilimia 18.5 la mapato ya ndani sio kidogo, Menejimenti fungeni mikanda, hatutarajii kushuka hapo, kila idara ihakikishe inakusanya mapato kwa asilimia 100" alisisitiza Mhe. Makaga huku akiwaomba madiwani hao kushirikiana na timu ya menejementi ili kufikia lengo la mapato.

Mbali na kupongeza bajeti hiyo, Baraza la Madiwani pia limeagiza menejimenti ya Halmashauri kuhakikisha wanawachukulia hatua kali wote wanaokwepa kulipa ushuru na tozo mbalimbali za Halmashauri.

Diwani wa kata ya Nyampande Mhe. George Kazungu amewaomba viongozi kuwa mfano bora kwenye ulipaji wa mapato ya Halmashauri ili iweze kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi na amesisitiza uwepo wa takwimu sahihi za wafanayabiashara wanaotakiwa kulipa leseni za biashara katika mwaka husika.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Sengerema ndugu Jamary Athuman amelipongeza baraza hilo na timu ya menejimeti kwa ushirikiano mzuri uliopo baina ya Serikalia na CCM ambapo kumeifanya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ipige hatua hivyo amelitaka baraza hilo kwenda kwa wananchi kiwaelezea mambo mazuri yanayotekelezwa na Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ndugu Binuru Shekidele amelishukuru baraza hilo kwa kukubali kupitisha mapendekezo hayo ya bajeti na ameahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na baraza hilo.

Mapema akiwasilisha mapendekezo ya bajeti, afisa mipango wa Halmashauri ndugu Pastory Mukaruka amesema bajeti inayopendekezwa imeongezeka kwa asilimia 1.12 kutoka shilingi 55,505,703,000.00 ya mwaka 2022/2023 na kufikia shilingi 56,136,022,839.00. Katika bajeti hiyo Mishahara ni shilingi 38,583,256,000.00, Ruzuku ya matumizi mengineyo ni shilingi 1,115,111,000.00, Ruzuku ya miradi ya maendeleo shilingi 7,025,121,000.00 na Ruzuku ya Wafadhili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 6,032,206,000.00



# MILIONI 73 ZANUFAISHA VIKUNDI 19 SENGEREMA

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Mkoani Mwanza imetoa Mkopo wa Shilingi Milioni 73 kwa vikundi 19 vya Wanawake shilingi milioni 42.5, Vijana shilingi milioni 25 na Wenye ulemavu shilingi milioni 6.5 vinavyojishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Akifungua mafunzo kwa vikundi vilivyonufaika na Mkopo huo (jumanne tarehe17 Januari, 2023) ndugu Boniphace Kasasiro kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji amesema mikopo hiyo isiyo na riba imetolewa na Halmashauri kwa vikundi hivyo kwa kufuata vigezo vyote, hivyo amewaomba wanavikundi hao kwenda kuitumia vyema kama ikivyokusudiwa na iweze kutimiza malengo ya wanavikundi hao.

"Tunavyo vikundi vingi vilivyosajiliwa katika Halmashauri yetu ambavyo viliomba Mkopo huu, hivyo ni vyema na ninyi mkirejesha mikopo hii kwa wakati ili vikundi vingine pia viweze kunufaika kama ninyi" amesema ndugu Kasasiro

Mapema akimkaribisha Mkurugenzi Mtendaji kwenye mafunzo hayo, Mwenyekiti wa jukwaa la Wanawake Sengerema Bibi Daling Matonange ameishukuru Halmshauri ya Wilaya ya Sengerema kwa kuongeza kiwango cha mkopo kwa vikundi hivyo ukilinganisha na kipindi kilichopita ambapo itavisaidia vikundi hivyo kufikia malengo na ndoto zao za kuwa wafanyabiashara wakubwa pamoja na kuzalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu.

Baadhi ya wanavikundi walionufaika na mkopo huo wameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa kutoa mikopo hiyo sambamba na kuwapa mafunzo ya namna bora ya kutumia fedha hizo kwani hapo awali waliogopa kuchukua mikopo hiyo kutokana na kutokuwa na elimu ya uelewa hivyo mafunzo hayo yatawasaidia kusimamia vyema fedha hizo pamoja na kufanya marejesho kwa wakati.

"Nimepata Mkopo kwa mara ya kwanza, kwa kiasi kikubwa mkopo huu umenimeongezea mtaji wangu ambao ulikuwa kidogo sana" amesema ndugu Sanifu Tanzania ambaye ni mnufaika kupitia kundi la wenye ulemavu.

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kutoa mikopo isiyokuwa na riba zaidi ya shilingi milioni 176 itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa vikundi mbalimbali vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.



# SEKONDARI SENGEREMA ZAPONGEZWA KWA UFAULU

Kufuatia shule za Sekondari za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kufanya vizuri kwenye matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne 2022, Mkurugenzi Mtendaji Ndg. Binuru Shekidele ametoa pongezi kwa idara ya elimu Sekondari, Walimu, Wahitimu wa kidato cha nne 2022, Wazazi pamoja na Wadau wote wa Elimu kwa matokeo mazuri ambapo ufaulu umekuwa wa asilimia 89.96.

Kupitia taarifa kwa umma iliyotolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imeweza kupata wanafunzi 778 kati ya 4095 watahiniwa wote wameafulu kwa daraja la kwanza ambapo pia shule tatu za Serikali ambazo ni Nyampulukano, Mwabaluhi na Kilabela zimeweza kufuta dara ja sifuri.

Kwa mujibu wa Matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani nchini (NECTA), jumla ya shule 38 za Serikali na binafsi zilizofanya Mtihani huo zilipata matokeo yafuatayo; Wanafunzi 337 wamepata ufaulu wa daraja la kwanza, Wanafunzi 778 wamepata ufaulu wa daraja la pili, Wanafunzi 777 wamepata ufaulu wa daraja la tatu, wanafunzi 1792 wamepata daraja la nne na wanafunzi 405 sawa na asilimia 10.03 ya watahiniwa wote wamepata daraja sifuri.

Aidha taarifa hiyo imebainisha kuwa Shule tatu za Chinfunfu, Kahumulo na Lusikwi zimeongeza ufaulu na kubakiwa na mwanafunzi mmoja aliyepata daraja sifuri. Shule zingine ambazo zimefaulisha vizuri na kupunguza daraja sifuri ni Nyancheche, Ngoma, Nyamahona na Nyamtelela.

Kwa mwaka 2022 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ilikuwa na jumla ya Watahiniwa 4,095 kwa shule zote 38 zilizoshiriki Mtihani huo.




# WAZAZI SENGEREMA WATAKIWA KUPELEKA WATOTO SHULE

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima amewataka wazazi wilayani Sengerema kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2023 wanakwenda kuanza masomo ifikapo jumatatu ya tarehe 16 Januari, bila kuwepo na visingizio vyovyote.

Mkuu wa Mkoa ametoa agizo hilo Jumamosi Januari 14, 2023 wakati wa hafla ya makabidhiano ya vyumba vipya vya Madarasa 152 iliyofanyika shule ya Sekondari Nyampulukano ambapo Mhe. Malima amekagua na kupokea madarasa matano kwa niaba ya mengine yaliyojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

"Wazazi hakikisheni watoto wote wanapelekwa shule kufikia Jumatatu (Januari 16, 2023) na mwisho kabisa jumanne lakini mzazi atayefika jumatano hajapeleka mtoto shule atakua ananitafuta, na namna pekee ya kumshukuru Mhe. Rais ni kuhakikisha watoto wanasoma kupitia madarasa haya mazuri aliyotujengea." Amesisitiza Mhe. Malima.

Kwa upande mwingine Mhe. Malima amewapongeza wazazi waliojitolea kuchangia ujenzi wa matundu ya vyoo 21 katika shule ya Sekondari ya Nyampulukano ambapo yeye pamoja na viongozi wengine wamechangia kiasi cha shilingi milioni 3 kwa ajili ya kuunga mkono juhudi hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amesisitiza juu ya agizo alilolitoa tarehe 28 Disemba, 2023 kuhusu watoto kwenda kujiunga kidato cha kwanza 2023 ambapo amesema hayuko tayari kusubiri miezi mitatu ifike ndiyo aanzishe zoezi la kusaka watoto ambao hawajaripoti shuleni, bali zoezi hilo litaanza tarehe 16 Januari 2023 na kuwataka wazazi kuwapeleka haraka watoto hao pasipo kuwepo na visingizio.

Katibu Tawala Mkoa, Ndugu Balandya Elikana ametoa shukrani kwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza kwa wakati mmoja kutokana na fedha alizotoa kujenga vyumba vya Madarasa na miundombinu yake ambavyo, hivyo ametoa wito kwa watoto kuendelea kuripoti shuleni kutumia fursa hiyo adhimu.

Akitoa taarifa ya Ujenzi wa madarasa hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Binuru Shekidele amesema kukamilika kwa vyumba hivyo kutachochea ufaulu kwa wanafunzi kwenye mitihani ya kitaifa.

Halmashauri ya wilaya ya Sengerema imekamilisha Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 152 gharama ya shilingi Bilioni 3.04 kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023 ambapo jumla ya wanafunzi 9451 waliofaulu wanaendelea kusajiriwa katika shule hizo



# SENGEREMA WASAINI MIKATABA KUONGEZA UFAULU SHULENI





Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kupitia Idara za Elimu Msingi na Sekondari mnamo tarehe 18 Januari, 2023 wamesaini mkataba na Maafisa Elimu Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema pamoja na wasaidizi wao yenye lengo la kuinua kiwango cha Elimu katika ngazi ya shule pamoja na kuongeza ufaulu shuleni.

Hafla hiyo ya usainiaji wa mikataba hiyo imefanyika Sekondari ya Sengerema ambapo kupitia mikataba hiyo, maazimio na vigezo kuhusu uboreshaji wa Elimu nchini imewasilishwa na kusainiwa na pande zote mbili.

Kusainiwa kwa mikataba hiyo ni ishara ya makubaliano ya kutimiza maazimio yaliyowekwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI).



# RC MALIMA ATAKA UWEPO MAJI YA UHAKIKA VITUO VYA AFYA NA SHULE

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa kuhakikisha huduma za Maji ya uhakika zinapatikana kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya pamoja na taasisi zote za elimu ili kupunguza adha kwa watoa huduma, wagonjwa, wanafunzi wa bweni pamoja wananchi wanaozunguka taasisi hizo.

Akikagua maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha afya Kanyelele kilichopo kata ya Buzilasoga kinachotarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 1852 chini ya Mpango wa kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) kwa zaidi ya Milioni 543, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima amesema huduma za afya haziwezi kutolewa pasipo kuwepo na huduma ya maji ya uhakika hivyo ameagiza kutengwe fedha ili kuchimba kisima kirefu kitakachosaidia kituo hicho pindi kitakapo anza kutoa huduma pamoja na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

"Kituo cha Afya bila huduma za maji haiwezekani na tusidanganyane na kutegemea Chanzo cha Maji ya mvua badala yake naomba Halmashauri itenge angalau Milioni 30 hapa ili tupate kisima kirefu cha Maji kwenye kituo hiki." Amesema mhe. Malima.

Aidha, mhe. Malima ameuagiza uongozi wa Halmashauri kuona namna kuongeza muda wa kufanya kazi na wafanyakazi kwenye kituo hicho ili kiweze kukamilika ifikapo Machi 15, 2023 ambapo amesema kukamilika kwa wakati kwa mradi huo pamoja na mingine ya TASAF kutasaidia kutimiza vigezo vya kuendelea kupata ufadhili wa miradi mingine ya maendeleo.

Mratibu wa TASAF wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ndugu Malisa Ndugha amesema ujenzi wa kituo hicho cha Afya Kanyelele umefikia Asilimia 80 na kinatarajiwa kuukamilika ifikapo Machi 10, 2023.

Miradi mingine iliyotembelewa na Mkuu wa Mkoa ni pamoja na Zahanati ya Mami, Shamba la mkulima mwezeshaji wa Pamba la ndugu Maneno Lukubanija wa Buyagu, Ukaguzi wa eneo la makazi ya wananchi watakaopisha eneo la Mgodi wa Nyanzaga, ujenzi wa vyumba saba vya madarasa Sekondari ya Ngoma pamoja na mkutano wa hadhara na wananchi wa Ngoma.






## SENGEREMA KUNUFAIKA NA SHULE 2 MPYA KUPITIA SEQUIP NA BOOST

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema itanufaika na ujenzi wa shule mbili mpya za Msingi na Sekondari kupitia Mpango wa Kuimarisha na Kuboresha Elimu ya Msingi nchini (BOOST) na Mpango wa Maendeleo wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) inayofadhiliwa na Benki ya dunia.

Hayo yamebainishwa tarehe 21 Machi, 2023 na timu ya ufuatiliaji kutoka Benki ya Dunia, TAMISEMI na Wizara ya Elimu wakati wa ziara ya siku moja ya kukagua maendeleo ya Mpango wa BOOST na SEQUIP kwa shule za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Kupitia ziara hiyo, Mkurugenzi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka TAMISEMI ndugu Susana Nyarubamba ameuagiza uongozi wa kata ya Misheni na Nyampukanomahali ambapo shule hizo zinajengwa, kuhakikisha miradi hiyo inajengwa kwa kufuata taratibu pamoja na ushirikishwaji wa wadau wote mhimu ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.

"Niwaombe ndugu zangu tufanye kazi kwa kushirikiana pindi miradi hii itakapoanza, asiwepo mtu wa kufanya kazi peke yake, tuzingatie maelekezo bila kukiuka taratibu, tufuate miongozo na maelekezo ya Serikali, tusipunguze thamani na ubora wa miradi hii" amesisitiza ndugu Nyarubamba.

Naye mwakilishi wa Benki ya Dunia ndugu Innocent Mulindwa mbali na kupongeza usimamiaji mzuri wa malengo ya BOOST na SEQUIP ameuasa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kuhakikisha wanaunga mkono juhudi za Serikali kupitia miradi hiyo kwa kusimamia vyema miradi hiyo ili thamani ya fedha iweze kuonekana.

Awali akisoma taarifa ya Halmashauri, Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi ndugu Donati Bunonos amesema Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inaendelea kutekeleza mpango wa BOOST na SEQUIP kupitia mpango wa mafunzo kazini kwa walimu wote (MEWAKA), ambapo kila shule imetenga masaa mawili kwa wiki lengo ikiwa ni kujengeana uwezo na umahiri wa kufundisha mada mbalimbali za masomo zinazoonekana kuwa na changamoto.

Kupitia mradi wa SEQUIP Halmashauri pia umefanikiwa kujenga shule mpya ya Sekondari ya Ibondo na vituo viwili vya mafunzo nje ya mfumo rasmi (AEPW) pamoja na utekelezaji wa mpango wa shule salama kwa shule zote za Sekondari.

Mpango wa BOOST na SEQUIP inatekelezwa katika Halmashauri zote nchini ikiwa na lengo la kuboresha na kuimarisha miondombinu ya shule, kuboresha mafunzo kazini ya walimu, kuongeza vifaa vya kufundishia na maabara.

Timu hiyo ya ufuatiliaji imetembelea shule ya Msingi Pambalu, Sekondari ya Ibondo, TRC Sengerema,Sekondari ya Nyampulukano, pamoja na maeneo ambapo shule mpya ya Sekondari ya kata ya Misheni itajengwa na kijiji cha Mwabayanda ambako kutajengwa shule mpya ya msingi kupitia mpango wa BOOST.



## CHITANDELE KUNUFAIKA NA NYUMBA ZA WALIMU KUPITIA TASAF

Shule shikizi ya Chitandele iliyopo kata ya Chifunfu imeanzisha ujenzi wa nyumba moja ya familia mbili (two in one) kwa ajili ya walimu wa shule Hiyo inayojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kwa kushirikiana na wananchi waliopo kisiwani humo.

Akiongea na wananchi mara baada ya zoezi la uchimbaji wa msingi wa nyumba hiyo, Diwani wa kata ya Chifunfu mhe. Robert Madaha amewaomba wananchi hao kujitoa kikamilifu kwa kushiriki katika ujenzi wa nyumba hiyo kwa kuchangia nguvu kazi ili nyumba hiyo ukamilike kwa wakati na walimu waweze kuishi karibu na shule hiyo.

"Tumepata bahati ya kuletewa mradi huu wa nyumba katika eneo letu, ni jambo jema kwetu hatuna budi kujitolea kwa nguvu kazi ili tukamilishe kwa wakati.

Akiongea kwa niaba ya Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri, Ndugu Neema Sagwa amewapongeza wananchi hao kwa kujitolea nguvu kazi ambapo amesema kuongeza kwa miundombinu katika shule hiyo shikizi kutasaidia kupata vigezo kwa ajili ya kuisajili na kuwa shule kamili ya msingi hivyo amewaomba wazazi wa eneo hilo kuhakikisha wanaandikisha watoto wote waliofikisha umri wa kwenda shule.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ndugu Malisa Ndugha amesema ujenzi wa nyumba hiyo unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi 68,760,943 fedha kutoka TASAF pamoja na nguvu za wananchi zinazokadiriwa kufikia shilingi milioni 6. Ndugu Malisa mesema ujenzi wa nyumba hiyo unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili 30, 2023 hivyo amewaomba wananchi hao pamoja na kamati ya ujenzi kuhakikisha wanatanguliza uzalendo kwanza katika shughuli za ujenzi wa nyumba hiyo.

Shule shikizi ya Chitandele ina jumla ya wanafunzi 100 wa darasa la awali hadi la nne, wanafunzi 13 wa darasa la tano hadi la saba waishio kisiwani humo hulazimika kwenda kusoma shule ya msingi Lukumbi iliyopo nje ya kisiwa hicho.

Kukamilika kwa nyumba hiyo kutaisadia shule hiyo shikizi hiyo kuwa na nyumba 2 za walimu ambapo kwa sasa kuna nyumba moja ya mwalimu.

Kisiwa cha Chitandele kilichopo kijiji cha Lukumbi kata ya Chifunfu kinakadiriwa kuwa kaya 76 na wakazi 300.



# Serikali Kuendelea Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma

Mhe. Jenista Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora amewapongeza watumishi wa umma kwa kujituma katika kuwahudumia wananchi na kuhakikisha wanamsaidia Mhe. Rais kutimiza ndoto ya kuwafikishia watanzania huduma bora katika nyanja zote.

Ametoa pongezi hizo mapema leo februari 21, 2023 wilayani Sengerema alipokua akizungumza na watumishi wa wilaya hiyo akiwa katika muendelezo wa ziara yake Mkoani Mwanza ambapo anakagua miradi iliyo chini ya wizara yake husussani inayotekelezwa na TASAF.

"Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala bora inashughulikia malimbikizo ya mishahara maana ni haki yao na wenye madai halali wote watalipwa,na zaidi ya Watumishi laki mbili wamepandishwa madaraja ndio maana hivi sasa tunahakikisha mtu akipandishwa daraja anaanza kupata mara moja mshahara wake mpya na hiyo ndio kiu ya Rais Samia katika eneo hili la utumishi." Waziri Mhagama.

Vilevile, amebainisha kuwepo kwa watumishi wa umma wanaoiangusha Serikali na ndio maana kuna ubadhirifu wa fedha za umma pamoja na usimamizi mbovu wa miradi hivyo amewasihi kuwajibika bila kusubiri kusukumwa kuhakikisha wanafanya kazi kizalendo ili kujenga uchumi wa nchi wa wenyewe.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amempongeza Mhe. Rais kwa kuwajali wanasengerema kwa kutekeleza Miradi ya Kimkakati kama Ujenzi wa Daraja la Kigongo- Busisi ambalo amesema litakapokamilika litasaidia sana kukuza uchumi wa wananchi wa Sengerema na Tanzania kwa ujumla.

Dkt. Angelina Samike, Mjumbe wa baraza Kuu la Shirikisho la vyama vya Wafanyakazi nchini ametaja changamoto ya uhaba wa watumishi na ametoa ombi kwa Serikali kuendelea kuongeza mshahara ya watumishi ili kuendana na hali ya uchumi kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa.

"Tunamshukuru sana Mhe. Rais Samia maana ametuheshimisha wafanyakazi kwa kutupandisha madaraja, kutupunguzia kodi na kuongeza kima cha chini cha mshahara, kutuongezea Mshahara, ametuboreshea mazingira ya kazi kwa kujenga nyumba za watumishi katika sekta ya Elimu na Afya na tunamwombea kwa Mungu afya njema." Amesema Dkt. Samike.



## BARAZA LA MADIWANI SENGEREMA LAKOSHWA NA UKUSANYAJI WA MAPATO

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema limeipongeza timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa kusimamia vyema zoezi ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kusimamia vizuri upelekaji wa fedha za asilimia 40 za miradi ya maendeleo zitokanazo na mapato hayo.

Wakiongea kwa nyakati tofauti kwenye kikao cha Baraza hilo kilichofanyika jumatano tarehe 15 Machi, 2023, wajumbe hao wamesema kwa sasa ukusanyaji wa mapato unakwenda vizuri hivyo wameitaka timu ya Menejimenti kuhakikisha inabuni vyanzo vingine vya mapato ikiwemo uboreshaji wa stendi ya Mabasi ya Bukala na ile ya Mnadani pamoja na soko la Migombani ili kufikia lengo la ukusanyaji mapato ya ndani.

Madiwani hao wamesema kitendo cha kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato kunarahisisha shughuli mbalimbali za Halmashauri zikiwemo za ujenzi wa miradi inayotegemea mapato ya ndani na shughuli zingine za utoaji huduma kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Mhe. Yanga Makaga amesema kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mambo mengi yanakwenda vizuri hivyo amewapongeza watumishi kwa kufanya kazi kwa kujituma na amewaomba madiwani kutoa ushirikiano ili kuweza kufikia malengo ikiwemo ukusanyaji wa mapato ya ndani.

"Halmashauri yetu kwa sasa imetulia, shughuli zinafanyika vizuri, ni vyema tuwe na tabia pia ya kuwapongeza watumishi wanapofanya vizuri" ameongeza kusema Mhe. Makaga.

Diwani wa kata ya Kahumulo ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira mhe. Fortunatus Nzwagi amesema kuna haja ya kuipongeza Menejimenti kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwani kwa kufanya hivyo kumesababisha upelekaji wa fedha za miradi inayotokana na mapato ya ndani kufika kwa wakati.

Naye diwani wa kata ya Tabaruka mhe. Sospiter Busumabu amesema Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa sasa mambo mengi yanakwenda vizuri hivyo ameliomba Baraza hilo kumpongeza Mwenyekiti wa Halmashauri kwa usimamizi mzuri wa Halmashauri ikiwemo ukusanyaji wa mapato ya ndani na usimamizi miradi mbalimbali ya Halmashauri.

Hata hivyo diwani wa kata ya Igulumuki ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya Elimu mhe. Deus Ndaki ameipongeza Idara ya Elimu Sekondari kwa kusimamia vizuri taaluma kitendo kilichopelekea kuongezeka kwa ufaulu kwenye mtihani wa kidato cha nne 2022 na kupunguza daraja sifuri kwenye baadhi ya shule.

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kukusanya shilingi 2,043,228,000 za mapato ya ndani, ambapo hadi sasa kufikia mwezi Februari 2023 imekusanya shilingi 1,204,751,966.19 sawa na asilimia 58.96 ya lengo la mwaka,



# WATENDAJI KATA SENGEREMA WANUFAIKA NA PIKIPIKI

Jumla ya watendaji 8 wa kata za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema wamenufaika na pikipiki zilitolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mzikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa lengo kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa maofisa hao.

Akikabidhi pikipiki hizo, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amewataka watendaji hao kutumia vizuri Pikipiki hizo ili ziweze kufikia malengo yalikusudiwa na Serikali ikiwemo ukusanyaji wa mapato pamoja utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

"Pikipiki hizi zimenunuliwa kwa kodi za wananchi, ni imani yangu mtazitumia vizuri tena kwa shughuli za Serikali" amesema Mhe. Ngaga.

Katika hatua nyingine Mhe. Ngaga ameliagiza jeshi la Polisi wilayani Sengerema kuhakikisha watendaji hao waliopewa Pikipiki wanapewa mafunzo ya namna bora ya utumiaji wa Pikipiki hizo na amewaagiza watendaji hao kuhakikisha wanakuwa na leseni za kutumia vyombo hivyo.

Mhe. Ngaga ameishukuru Serikali kwa kuwajali watumishi ambapo amesema ndani ya mwaka mmoja Serikali imetoa Pikipiki 83 kwa watumishi wakiwemo maafisa kilimo na watendaji wa kata za Halmashauri ya Sengerema na Buchosa

Mapema akimkaribisha Mkuu wa Wilaya kukabidhi Pikipiki hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Binuru Shekidele amesema Pikipiki hizo kwa awamu hii ya kwanza zimetolewa kwa watendaji wa kata za pembezoni kwa lengo la kuwasaidia kutimiza majukumu yao ya kila siku ikiwemo ukusanyaji wa mapato.

Mtendaji wa kata ya Chinfunfu Emmanuel Ng'alalile ameishukuru Serikali kwa kuwasaidia usafiri ambapo amesema umbali kutoka kata hiyo hadi makao makuu ya Halmashauri ni zaidi ya kilomita 50 hivyo itamsaidia katika majukumu yake ya kila siku ikiwemo upelekaji wa taarifa za ofisi pamoja na utoaji wa huduma kwa wakati.

Pikipiki hizo 8 zimekabidhiwa kwa watendaji wa kata za Chinfunfu, Igalula, Kagunga, Buyagu, Kasenyi, Buzilasoga, Igulumuki, na Ngoma.



# BUYAGU KUWA KITUO CHA MFANO KILIMO CHA PAMBA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima amepania kuboresha kilimo cha zao la Pamba ambapo ameagiza kuanzishwa kwa umoja wa wakulima wa Pamba Buyagu Wilayani Sengerema ili kuongeza uzalishaji na kutoa elimu kwa wakulima wa maeneo mengine.

Akizungumza na baadhi ya wakulima wa Pamba wa kata ya Buyagu alipotembelea mashamba yao ya Pamba, Mhe. Malima amesema bado wakulima wa zao hilo hawalimi kilimo cha kisasa kitendo ambacho kinarudisha nyuma uzalishaji wa zao hilo, ambapo amesema mpango wa kuanzisha kilimo cha kisasa cha zao hilo utaenda sambamba na kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili watu wengine kutoka maeneo mengine wajifunze.

"Mimi ninataka wakulima wengine kutoka maeneo yote ya Afrika waje wajifunze Buyagu kilimo bora cha Pamba na inwezekana" amesisitiza mhe. Malima

Mkuu wa Mkoa ameiagiza Bodi ya Pamba kushirikiana na Halmashauri kuanzisha umoja wa wakulima wa Pamba wa eneo hilo pamoja na kujenga kituo maalumu cha wakulima wa Pamba kwa ajili ya kuwahudumia wakulima hao kitendo ambacho kitapelekea wakulima kuweza kukopeshwa Pembejeo.

"Mimi nawaomba, tutenge kanda hii iwe ya majaribio kwenye zao la Pamba. Tutafanya usajili wa wakulima wote, lazima tupime pia udongo huu tujue ni mbolea gani inahitajika" amesema mhe. Malima

Mhe. Malima amesema mpango huo pia utahusisha utoaji wa mikopo ya Pembejeo kwa kushirikiana na mabenki pamoja na Halmashauri kuwezesha miundombinu ya umwagiliaji pamoja na elimu ya upandaji kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo ili mkulima kwa hekari moja apate kilo angalau 2000.

Mkuu wa Mkoa amesikitishwa kutokana na kuwaona wakulima wakipoteza fursa ya kupata fedha nyingi kupitia zao la Pamba kutokana na kutokuzingatia kanuni bora za kilimo cha Pamba.

Mkuu wa Mkoa ameunda kamati maalumu inayohusisha wataalamu wa kilimo ngazi ya Wilaya na Mkoa ambapo itaandaa taarifa mhimu za wakulima hao pamoja na ukubwa wa mashamba yao.



# DC SENGEREMA AKEMEA MMOMONYOKO WA MAADILI

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amekemea tabia ya baadhi ya wazazi kujiweka kando kwenye malezi ya watoto kitendo kinachosababisha kushuka kwa maadili katika jamii.

Mhe. Ngaga ametoa angalizo hilo kwenye maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kiwilaya kwenye viwanja vya stendi ya zamani mjini Sengerema na kuhudhuriwa na mamia ya wanawake.

Mhe. Ngaga amesema wakinamama wanalo jukumu kubwa la malezi majumbani lakini kutokana na kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi na uzalishaji mali wamesahau kujihusisha na malezi hivyo amewataka wanawake hao kutimiza majukumu yao ikiwemo kufuatilia mienendo ya watoto wawapo majumbani na mahali pengine.

"Tunajukumu kubwa la malezi ndugu zangu, ni lazima tufuatilie watoto wetu wanakutana na changamoto gani kila siku, ni lazima tufuatilie na tujue watoto wetu wanakoenda wanakutana na changamoto gani?" amesisitiza Mkuu wa Wilaya.

Aidha Mhe. Mkuu wa Wilaya amewaasa wazazi kuwa makini na matumizi ya Teknolojia kwa watoto kwani mmomonyoko wa maadili kwa kiasi kikubwa umechangiwa na matumizi mabaya ya Teknolojia ikiwemo matumizi ya simu janja kwa watoto.

Katika upande mwingine Mkuu wa Wilaya amewataka wanawake wilayani Sengerema kuhakikisha wanashirikiana katika kuinua vipato vyao kupitia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali hususan mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kupitia Halmashauri za Wilaya kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vyenye lengo la kuwakwamua wanawake kupitia vikundi mbalimbali.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ndugu Christina Bunini akimkaribisha Mkuu wa Wilaya amewaasa wanawake hao kuhakikisha wanatimiza majukumu ya malezi ya watoto majumbani ili kuwa na jamii yenye maadili kwani akina mama wanayo nafasi kubwa ya kusimamia malezi bora katika ngazi ya familia.

Mapema akitoa taarifa ya maadhimisho hayo ndugu Boniphace Kasasiro amesema lengo la maadhimisho ya wanawake duniani ni pamoja na kufanya tathimini ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na akina mama pamoja na kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake.

Mwenyekiti wa Jukwaa la wanawake Wilayani Sengerema ndugu Daling Matonange ameiomba Serikali kupitia Halmashauri kuweza kuongeza kiwango na wigo wa mikopo kwa Burundi vya wanawake kwani vipo vikundi vingi ambavyo vinazalisha bidhaa mbalimbali ambavyo hukabiliwa na changamoto za kukosa mikopo hiyo.


HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
HERI YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI
KAULI MBIU
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema tunajivunia kuwa na viongozi na watumishi wanawake ambao wamekuwa chachu ya maendeleo ya Halmashauri hii
Ubunifu na Mabadiliko ya Technolojia : Chachu katika kuleta Usawa wa Kijinsia
sengeremadc
http://www.sengeremadc.go.tz/





# RC MALIMA ATIMIZA AHADI YAKE KWA WANANCHI WA MAMI

- **Mkuu wa Wilaya atoa siku 5 wazazi kupelekea watoto shule**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Kigoma Malima ametimiza ahadi yake ya fedha taslimu na mifuko 20 ya Saruji kwa wananchi wa kijiji cha Mami kilichopo kata ya Kishinda Wilayani hapa.

Akikabidhi fedha hizo shilingi laki 7 (laki 5 za Mkuu wa Mkoa, laki 1 kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya na laki 1 kutoka kwa mdau wa maendeleo wa Kishinda) leo tarehe 08 Machi, 2023 kwa wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amewapongeza wananchi hao kwa kujitolea kuchangia nguvu kazi kwenye miradi mbalimbali ambapo amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia miradi inayopelekwa katika eneo hilo kukamilika pasipokuwa na migogoro.

"Hiki mnachokifanya cha kujitolea ni kitu kizuri sana na cha kuigwa, ukichangia kwenye miradi ya maendeleo unakuwa na uchungu na mradi huo kwa sababu umechangia na mradi utauthamini" amesema Mkuu wa Wilaya.

Kwa upande mwingine Mkuu wa Wilaya ametoa siku 5 kwa mtendaji wa kata ya Kishinda kuhakikisha anawakamata wazazi wa watoto wote ambao hawajajiunga kidato cha kwanza katika shule za Sekondari Kishinda na Tunyenye akishindwa kufanya hivyo hatua kali zitachukuliwa kwa mtendaji huyo.

Diwani wa kata ya Kishinda Mhe. Vicent Shokolo ameipongeza Serikali kwa kupeleka miradi mingi katika kata hiyo ambapo amemhakikishia Mkuu wa Wilaya ya Sengerema kuwa, miradi yote itakayopelekwa katika kata hiyo wananchi wapo tayari kuchangia nguvu kazi kwani wanathamini jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kupeleka miradi ya maendeleo katika kata hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Binuru Shekidele amewapongeza wananchi wa kijiji cha Mami kwa kujitolea kuchimba mtaro kwa ajili ya kupeleka maji katika zahanati ya kijiji hicho ambapo amewaomba kuendelea na moyo huo wa kujitolea kwa miradi mingine.

Akiwa katika ziara yake Wilayani hapa tarehe 1 Machi, 2023 Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima aliahidi kuchangia shilingi laki 5 kwa ajili ya chakula cha wananchi wa kijiji cha Mami waliojitolea kuchimba mtaro wa kupitisha bomba la maji linalopeleka maji kwenye zahanati ya kijiji cha Mami pamoja na mifuko 20 ya Saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule ya Msingi Mami.



# SPORTS CHARITY YAPIGA TAFU VIFAA VYA MICHEZO SENGEREMA

Shirika la Sports Charity la jijini Mwanza leo ijumaa Februari 24, 2023 limetoa misaada ya mipira zaidi ya 300 kwa shule za Msingi na Sekondari za Halmashauri ya Sengerema ikiwa ni lengo la kuibua michezo mashuleni.

Akiongea wakati wa hafla ya makabidhiano ya Mipira hiyo Mkurugenzi wa shirika hilo Mwalimu Rogatian Kaijage amewaasa walimu wa michezo kuhakikisha mipira hiyo inakwenda kutumika shuleni ili kuweza kuinua kiwango cha michezo.

"Tunaimani mipira hii ambayo tunawapa leo itaenda kutumika vizuri, tuibue vipaji huko mashuleni" amesema Mwalimu Kaijage.

Katika hatua nyingine Mwalimu Kaijage amesema lengo la kugawa vifaa hivyo vya michezo ni pamoja na kuishawishi Serikali kuwekeza zaidi kwenye michezo kwani huko ndiko kuna vipaji hivyo ameshauri kitengo cha Michezo wilayani hapa kuhakikisha wanasimamia vyema programu mbalimbali za michezo kupitia kwenye vituo maalumu vya kukuzia vipaji vilivyopo Sengerema.

Akishukuru kwa niaba ya Halmashauri, Afisa michezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ndugu Fortunatus Masaga amelishukuru shirika hilo kwa kuamua kutoa vifaa hivyo ambavyo vitakwenda kuibua vipaji mbalimbali mashuleni hivyo amewaomba walimu wa michezo kuhakikisha wanatumia mipira hiyo kwa masilahi ya wanamichezo mashuleni.

Mipira iliyotolewa ni pamoja na ile ya Miguu, Mikono, wavu na Kikapu ambapo kila shule imepewa mipira miwili na vituo maalumu vya kukuzia vipaji vimepewa mipira ya miguu mitano na mkono mitano.

